



JAMHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA


MPANGO MKAKATI KUELEKEA UCHUMI WA KATI

HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

MKOA WA NJOMBE

Desemba 2016

RAMANI YA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE INAYOONESHA MIPAKA NA MAENEO YA UTAWALA



Dira

Dira ya Halmashauri ya mji Njombe ni ***“Kuwa na Jamii yenye maisha bora na maendeleo endelevu ifikapo 2025”.***

Dhima

Dhima ya Halmashauri ya Mji Njombe ni ***“Kutumia fursa na rasilimali zilizopo kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo kutoa huduma bora na endelevu kwa jamii kwa kuzingatia uzalendo na misingi ya utawala bora***

DIBAJI

Halmashauri ya Mji Njombe imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali Kuu, Dira ya maendeleo ya Taifa – 2025, Malengo ya Maendeleo endelevu (SDGs), Mkakati wa Taifa wa kuondoa umaskini na kukuza uchumi (MKUKUTA), Sera na Malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Miongozo hii yote imeweka mikakati ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea Mageuzi ya Uchumi na maendeleo ya watu kama ilivyotafsiriwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 -2020/2021).

Hivyo ili halmashauri iweze kufikia malengo ya kuwa katika uchumi wa kati ni lazima kujizatiti katika mikakati itakayochochea ukuaji wa sekta za kilimo na viwanda. Kwa kuwa Halmashauri yetu kijiografia ina fursa nyingi ukilinganisha na sehemu zingine (comparative advantage) kuweza kukuza sekta ya viwanda hasa vinavyozalisha bidhaa zitokanazo na mali ghafi za kilimo na mifugo, juhudi kubwa zimeelekezwa katika kuimarisha ushiriki na ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi (Public Private Partnership).

Jukumu kubwa la Halmashauri ya Mji Njombe ni kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuwekeza katika nyanja mbalimbali hususani katika uzalishaji wa mazao ya kilimo (Mashamba makubwa), Viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vitavyoweza uchakataji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani na pia uwezesaji wa sekta binafsi ziweze kutoa huduma mbalimbali kwa wazalishaji wengine pamoja na wananchi kwa ujumla.

Hivyo halmashauri katika mkakati huu imejielekeza zaidi katika kubainisha fursa zitakazoweza sekta ya kilimo kuongeza uzalishaji, kutoa fursa za uwekezaji katika viwanda vya uchakataji na ardhi/miundombinu ambazo hatimaye kuchochea ajira kwa wananchi wengi na ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Kwa kifupi fursa za kiuchumi zilizopo, Mikakati iliyowekwa na hatua za kimkakati zilizopangwa zimeainishwa katika mpango mkakati huu.

**I.L Mwenda
Mkurugenzi
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE**

MPANGO MKAKATI WA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE KATIKA KUELEKEA UCHUMI WA KATI

1.0 Utangulizi

Halmashauri ya Mji Njombe ni moja kati ya Halmashauri tatu (3) zinazounda Wilaya ya Njombe, Halmashauri nyingine ni Mji Makambako na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Halmashauri hii ilianzishwa mwaka 2007 baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kugawanywa. Kwa upande wa Mashariki imepakana na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Kaskazini imepakana na Halmashauri Wilaya ya Wanging'ombe, Magharibi imepakana na Wilaya ya Makete na Wanging'ombe, Kusini imepakana na Wilaya ya Ludewa na Mkoa wa Ruvuma. Halmashauri ya Mji Njombe ina ukubwa wa mita mraba 3,212 za eneo linalojumuisha Tarafa 2, Kata 13; Kata (3) ni za mjini na (10) ni za Vijijini, Vijiji 44 na Mitaa 28.

1.1 Idadi ya Watu

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Halmashauri ya Mji Njombe ilikuwa na watu wapatao 130,223 (Me 61,112 na Ke 69,111). Kwa mwaka 2016 idadi ya watu inakadiriwa kuwa 134, 801 (Wanawake 71,541 na Wanaume 63,260). Hii ni kutokana na ongezeko la ukuaji wa idadi ya watu la asilimia 0.8 kwa mwaka.

1.2 Hali ya hewa

Kwa jumla hali ya hewa ya Halmashauri ya Mji wa Njombe ni nzuri kwa maisha na uzalishaji. Kipindi cha mvua huanza Mwezi Oktoba hadi Aprili ambapo mvua hufikia kati ya milimita 1200 hadi 1400 kwa Mwaka. Aidha, baadhi ya maeneo hupata mvua za vuli katika kipindi cha mwezi Septemba. Aidha kuna kipindi cha baridi ambapo joto hushuka hadi (4⁰C) kipindi hiki huanza mwezi Mei hadi Agosti; na kipindi cha majira ya joto (28⁰C) huanza mwezi Novemba hadi Machi.

2. Hali halisi na fursa za maendeleo kiuchumi na kijamii

2.1 Sekta ya Kilimo na ushirika

Sekta ya kilimo kama ilivyo kwa nchi nzima ndio uti wa mgongo wa uchumi wa wananchi wa Halmashauri ya Mji Njombe. Asilimia 77.9% ya wananchi wa Halmashauri ya Mji Njombe wanategemea kilimo katika kuendesha maisha yao. Ardhi inayofaa kwa kilimo ni hekta 192,700 sawa na asilimia 59.9 ya ardhi yote. Kwa ujumla Halmashauri inazalisha chakula cha kutosha na ziada kwa takriban kila mwaka. Kwa msimu wa mwaka 2015/2016 uzalishaji wa mazao ya chakula ulikuwa tani 295,163; (Mahindi tani 114,018; Ulezi tani 254; Ngano 4,846; Viazi vitamu tani 3,738; Viazi mviringo tani 166,889; Maharage tani 3,584 na Njegere tani 1,834).

Aidha mazao ya biashara yaliyozalishwa kwa msimu wa mwaka 2015/2016 ilikuwa ni tani 30,531. (Chai tani 30,433; Maua tani 2; Alizeti tani 81; Pareto tani 34; Kahawa tani 6; Chemomile tani 4 na Papermint tani 1). Halmashauri imeendelea kuhimiza jamii katika kilimo cha matunda, ambapo kwa Mwaka 2015/16 mazao ya matunda yalikuwa ni tani 608. Matunda yaliyolimwa ni Apples, Peasi, Parachichi, Nanasi, Stafeli, Mabohora na Mapera.

Halmashauri imeendelea kupambana na changamoto zinazojitokeza kwa kutoa huduma za ugani/ushauri na kuhimiza jamii kutumia pembejeo bora za kilimo kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Kwa mwaka 2015/2016, Wakulima walitumia Jumla ya tani 65,890 za mbolea, lita 22,108 za madawa na tani 423 za mbegu bora. Kwa ujumla pato la mwananchi wa Halmashauri ya njombe linakdiriwa kuwa ni wastani wa shilingi 750,000 (NBS) kwa mwaka kiasi ambacho bado ni kidogo kulinganisha na fursa zilizopo.

2.2 Fursa zilizopo katika sekta ya kilimo

Katika kuelekea uchumi wa kati Halmashaurim ya Mji Njombe inazo fursa nyingi zinazotegemea uzalishaji uliopo kwa mazao ya kilimo hususani katika uongezaji thamani na ufungashaji mazao ya chakula, Matunda na mbogamboga. Hadi sasa (2016) halmashauri kupitia sekta binafsi inavyo viwanda vitatu(3) vidogo vya kusindika alizeti; kiwanda kimoja(1) kidogo cha kusindika unga wa mahindi; Kiwanda kidogo kimoja (1) cha kusindika Mikate; Kiwanda kidogo kimoja (1) cha kusindika matunda na Viwanda vikubwa viwili (2) vya Kusindika majani ya Chai. Kwa kuzingatia takwimu hizi bado fursa ya uwekezaji katika sekta ya kilimo ni kubwa kwani viwanda hivi havijafikia kiwango cha kutumia malighafi yote inayozalishwa na kuiongezea thamani ili kutwaa masoko ya ndani na nje. Mfano;- Matunda mengi yanaoza mashambani; mahindi, Nyanya na mbogamboga zinauzwa bila kuongezewa thamani

2.3 Sekta ya Mifugo

Pamoja na wakazi wa Mji wa Njombe kujikita kwenye kilimo pia shughuli nyingine ni ufugaji ambapo eneo lililotengwa kwa ajili ya ufugaji ni hekta 4,588 sawa na asilimia 1.4 ya ardhi yote. Kwa mwaka 2015 Halmashauri ilikuwa na jumla ya Ng'ombe 35,731; Mbuzi 18,548, Kondoo 3,740, Nguruwe 6,194, Punda 7,930 na Kuku 54,249. Kwa upande wa miundombinu ya mifugo, Halmashauri ina jumla ya majosho 12 (yanayofanya kazi ni 8), machinjio 2, Vibanda vya kuchinjia (slaughter slabs) 80, Vibanio vya kudumu 80, mnada wa mifugo 1 (unaendelea kujengwa) na kituo cha huduma za mifugo 1

2.4 Fursa zilizopo katika sekta ya mifugo

Ufugaji wa Ngombe wa kisasa bado uko chini na hivyo fursa ya hali ya hewa haijatumika vizuri kuweza kuongeza ufugaji, uzalishaji na usindikaji wa maziwa na mazao mengine ya mifugo. Pamoja na kuwepo kiwanda cha Maziwa cha CEFA bado kunahitajika uzalishaji uongezwe ili wananchi wengi waweze kunufaika na hivyo kuongeza uzalishaji katika viwanda hiki kwa ajili ya soko la ndani na nje. Aidha mazao mengine yatokanayo na mifugo bado uzalishaji na uongezaji thamani uko chini na hivyo fursa ya hali ya hewa haijatumika vizuri kuweza kuongeza ufugaji, uzalishaji na usindikaji wa maziwa na mazao mengine ya mifugo kama vile ngozi. Fursa za uzalishaji wa nyasi za malisho na chakula bora cha mifugo pia ni eneo jingine ambalo linahitaji msukumo ili kuimarisha afya ya mifugo

2.5 Elimu Ya Ufundi

Ndani ya Halmashauri ya Mji Njombe kuna shule za msingi 83 na 14 za sekondari zilizo na uwezo wa kutosha kutoa wanafunzi katika Vyuo hususani vya ufundi (VETA) na vyuo vingine pia. Vyuo vya ufundi ni muhimu katika kuwezesha vijana kuwa na ujuzi wa kufanya kazi na kujiajiri katika uzalishaji wa huduma mbalimbali za ufundi ambazo zinahitajika kwa kiwango cha juu katika viwanda vya kati, vikubwa na zaidi katika majenzi ya miundombinu mbalimbali kwa jamii. Ndani ya eneo la halmashauri ya Mji Njombe kuna vyuo vya ufundi stadi tisa (09) ambavyo bado havikidhi mahitaji kwa idadi ya vijana na wanachi wa Halmashauri

2.6 Fursa za uwekezaji zilizopo sekta ya elimu ufundi

Kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya sekondari na msingi ni Fursa kubwa kuweza kuwekeza katika vyuo vya ufundi ambavyo vitawezesha vijana kupata ujuzi na kuweza kujiajiri katika nyanja mbalimbali za uzalishaji mali. Halmashauri tayari imetenga eneo maalumu kwa ajili ya uwekezaji katika nyanja mbalimbali za ufundi stadi kwa SIDO na VETA. Aidha uwekezaji katika vyuo vya elimu ya juu nao unahitajika kwani kwa sasa kuna Tawi la Chuo kikuu huria na campus ya Amani ambalo ni tawi la Chuo kikuu cha cha Tumaini

2.7 Sekta ya Maji

Halmashauri ina jumla ya mitandao 83 ya kusambaza maji safi ('Gravity' 49, 'Hydrum' 31, Mchanganyiko 3). Aidha kuna jumuiya 10 za watumia maji zilizosajiliwa na jumuiya nyingine 6 zipo katika hatua mbalimbali za usajili. Kwa Mwaka 2016 Halmashauri ina jumla ya wakazi 78,733 (59%) wanaopata huduma ya maji. Halmashauri ya Mji Njombe imeongeza upatikanaji wa huduma ya maji Kutoka 39.5% mwaka 2009 hadi 50.5% mwaka 2016 Vijijini na maeneo ya Mjini kutoka 69.1% mwaka 2015 hadi 79.0% mwaka 2016.

Hata hivyo bado jitihada za kutekeleza sera ya maji zinaendelea kuapitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira ya taifa (NWSSP), kushirikiana na NJUWASA; Wafadhili kama ACRA, SHIPO, Roman Catholic(kiwanda cha Maji-

Lugenge) na wananchi kwa ujumla. Upatikanaji wa maji ya kutosha katika Halmashauri ya Mji Njombe ni cha umuhimu wa pekee kwani matumizi ya maji yanahitajika katika sekta zote zo kiuchumi na kijamii kwa ujumla. Uwepo wa Mito na chemichemi ni fursa ambayo wawekezaji na wananchi wanatakiwa kuitumia vizuri ikiwa ni kwa kutunza vyanzo vya maji na pia kuongeza thamani kwa kuanzisha viwanda vya kuyafungasha kwa ajili ya soko la ndani na nje kama inavyofanyika kwa sasa kupitia kiwanda cha maji cha Njombe chemichemi

2.8 Sekta ya Misitu

Miti ni kuu la biashara kwa wananchi katika halmashauri ya Mji njombe. Wananchi na wadau mbalimbali toka ndani na Nje ya halmashauri wamewekeza vya kutosha katika sekta hii ambapo inakadiriwa kwamba mashamba ya miti yapatayo hekta **85,702** (NTC, 2012) yanamilikiwa na wananchi na sekta binafsi kama TANWAT , LUPONDE, nk.Vilevile katika kutekeleza hifadhi ya mazingira kupitia kampeni ya upandaji miti Kitaifa, Halmashauri kwa mwaka 2015/16 imepanda jumla ya miti **11,356,265** kwa kushirikisha wadau mbalimbali.

2.9 Fursa zilizopo sekta ya misitu

Kutokana na uwepo wa malighafi ya mbao na miti ya kutosha katika Halmashauri ya Mji Njombe; wananchi na sekta binafsi wanahimizwa kuendelea kuwekeza zaidi katika uchakataji wa mazao ya misitu ili kuongeza thamani. Fursa zilizopo ni kuwa na viwanda bora vya mbao,samani na mazao mengineyo yatokanayo na mbao/magogo ya miti. Hii itaondoa utegemezi wa bidhaa za misitu toka nje ya Mkoa wa Njombe kwa wanchi wa Njombe na hata kuwezesha watanzania kupata samani toka Mkoa wa Njombe badala ya kununua toka Nje ya Nchi

2.10 Sekta ya Viwanda na biashara

Halmashauri ya mji Njombe pamoja na uchanga wake, inavyoviwanda mbalimbali vikubwa,vya kati na vidogovido vinavyomilikiwa na kuendeshwa na Mashirika, sekta binafsi na wakati mwingine kwa kushirikiana na halmashauri. Kuna viwanda vikubwa vitano **(5)** vikiwemo kiwanda cha kuchakata Mbao na Magogo**(1)** na Miwati **(1)** vyote vinamilikiwa na TANWAT Co.; Viwanda vya Chai LUPONDE na KIBENA, na Kiwanda cha Maziwa na Jibini (NMF Co.Ltd). Aidha kuna viwanda **(13)** vya kati ambavyo ni vya kusindika na kufungasha mazao kama vile mafuta **(3)**,unga wa Sembe**(3)** na Mchele**(2)**; Kiwanda cha Maji Nole/Ihalula **(1)** na Mbao na magogo **(4)**.

Pia kuna mashine/viwanda vidogovidogo **183**; kati yake mashine za kusaga na kukoboa nafaka ni (157), kukamua mafuta (3); viwanda vya mafundi seremala **(20)** na kuna machinjio**(3)**. Viwanda hivi vyote vinasaidia kukuza ajira kwa idadi kubwa ya wananchi wa Mji wa Njombe kuanzia ajira za utoaji huduma moja kwa moja na kwa wafanyabiashara wa jumla, rejareja na wachuuzi; Vibarua na

watumishi wa ajira za kudumu. Viwanda hivi kwa pamoja vinakadiriwa kuajiri wastani wa watu **1,698** sawa na asilimia **2.3** ya wakazi wa halmashauri ya mji wenye uwezo wa kufanya kazi

2.11 Fursa zilizopo Sekta ya Viwanda na biashara

Fursa iliyopo katika sekta hii ni uwekezaji katika viwanda vya kati na vikubwa ili kuongeza thamani kwa mazao ya kilimo na mifugo yanayozalishwa kwa wingi na wakulima na wafugaji kwani viwanda vilivyopo bado havijafikia uwezo wa kutumia malighafi yote inayozalishwa. Aidha wawekezaji waliopo wataendelea kuhamasishwa ili waweze kuongeza uwezo wa viwanda vyao ili kukidhi mahitaji ya soko na hivyo kupanua uzalishaji. Katika kuwezesha utekelezaji wa mkakati huu halmashauri ya Mji Njombe imetenga maeneo na kuyapima na mengine kuyatolea fidia ili kuwezesha wafanyabiashara ndogondogo kufanya biashara zao bila kubughudhiwa. Juhudi za kuimarisha miundombinu katika maeneo hayo zinaendelea kufanyiwa kazi kadri ya fedha za mapato ya ndani zinavyopatikana. Aidha dawati la ushauri na uwezeshaji sekta binafsi limeanzishwa ili kuboresha mawasiliano kati ya wawekezaji, wananchi na halmashauri.

2.12 Sekta Wezeshi

2.12.1 Uchukuzi na Mawasiliano

Halmashauri ina mtandao wa barabara zenye urefu wa Km 1,392 (Km 160 za lami, Km 172 za changarawe na Km 1,060 ni za udongo) Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016 Halmashauri imeweza kuzifanyia matengenezo barabara za changarawe zenye urefu wa km 247, udongo km 350 na lami km 8.6. Pia madaraja 35 ya zege yamejengwa katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Mji Njombe. Kwa wastani eneo la Halmashauri ya mji wa Njombe linapitika kwa barabara za changarawe na udongo na limeunganishwa na mikoa mingine kwa barabara kuu za lami na kiwanja cha ndege ambacho kinatumika kwa ndege ndogo. Hivyo usafiri na usafirishaji wa bidhaa za misitu, mazao ya kilimo na bidhaa zingine ni mzuri.

2.12.2 Sekta Ya Nishati na Mawasiliano

Chanzo kikuu cha nishati ya umeme katika Halmashauri ya mji Njombe ni umeme unaosambazwa na shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) hususani katika kata zake tatu za Njombe Mjini, Ramadhani na Mjimwema. Pamoja na TANESCO, kuna Mashirika mengine yanayotoa huduma ya Umeme ni TANWAT, Roman Catholic Mission katika vituo vya Uwemba na Imiliwaha. Kwa maeneo ya nje ya mji, Vijiji 17 viko katika mpango wa kupatiwa umeme kupitia programu ya Umeme vijijini (REA) vijiji hivi ni pamoja na Peruhanda, Idunda, Igominyi, Iboya, Lwangu, Itipula, Ihanga, kifanya, Lilombwi, Liwengi, Mikongo, Lwangu, Yakobi, Magoda, Madobole, Dansland na Kona.

Aidha Ujenzi wa Msongo Mkubwa (HT) unaendelea toka Makambako – Madaba – Songea na unatarajiwa kukamilika Mwezi Desemba 2016 na baadae kufuatiwa na ujenzi wa vituo vya kupooza umeme kwa ajili ya usambazaji kazi ambayo kwa Halmashauri ya Mji Njombe itafanywa na TANESCO na REA. Pindi kazi hii itakapokamilika itarahisisha na kuharakisha uwekezaji katika maeneo mbalimbali yaliyoainishwa kwa kwa uwekezaji na hivyo kuongeza tiza zaidi.

Kwa upande wa mawasiliano Halmashauri ya Mji Njombe imeunganishwa na Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa. Makampuni ya simu ya TTCL na TTCL Mobile, TIGO, VODACOM na AIRTEL yanatoa huduma za mawasiliano kwa sehemu kubwa ya halmashauri na hivyo kuboresha huduma zingine zinazotegemea mawasiliano. Vilevile kuna vituo vya matangazo ya radio vya Uplands FM, KISS FM, RFA, TBC Taifa, Ebony FM na zingine nyingi zilizo nje ya halmashauri na Mkoa zinapatikana pia.

2.12.3 Fedha

Huduma za kifedha zinapatikana na zinatolewa na bank za CRDB, NMB, NBC, Bank ya Posta, na Bank ya wananchi wa Njombe (NJOCOA). Vile vile kuna vyama vya kuweka na kukopa (SACCOSS na VICOA), FINCA n.k katika maeneo ya mjini na vijijini ambavyo navyo vinawezesha wananchi kupata huduma za kifedha kulingana na mahitaji yao.

2.12.4 Sekta ya Ardhi na mipango miji

Katika mwaka 2015/16 Halmashauri ya Mji wa Njombe imepima viwanja 313 na kuwezesha upatikanaji wa hati miliki 202 na kumilikishwa kwa wananchi na taasisi. Aidha katika kuboresha mpango na uendelezaji wa ukuaji wa mji wa Njombe Halmashauri inaandaa mpango kabambe (Master plan) ambao tayari uko hatua ya ukusanyaji takwimu za awali za kiuchumi na kijamii na baadae maandalizi ya michoro yafanyike kwa kuzingatia mahitaji ya huduma za jamii. Mpango huu utawezesha halmashauri ya mji Njombe kuwa katika mandhari iliyopangiliwa vizuri katika matumizi ya ardhi na kuepusha migogoro ya ardhi isiyo ya lazima pindi utakapokamilika.

2.12. 5 Afya

Halmashauri ina jumla ya vituo 58 vya kutolea huduma; hospitali 2 (1 inamilikiwa na Serikali na nyingine kampuni ya TANWAT), Vituo vya Afya 8 (1 Serikali, 5 mashirika ya dini na 2 watu binafsi) na Zahanati 48 (42 za Serikali, 3 mashirika ya dini na 3 watu binafsi). Pia Halmashauri kwa kushirikiana na Wananchi inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi na uboreshaji wa Zahanati **13 (Ng`elamo, Iboya, Iwungilo, Mtila, Itulike, Kitulila, Lusitu, Mbega, Nole, Mfereke, Matalawe, Utalingolo, na Kituo cha Afya cha Kifanya)** ambapo

zitakapokamilika zitaboresha zaidi utoaji wa huduma za afya na hivyo kufikia malengo ya serikali ya kuwa na zahanati kila kijiji kwa 100%.

Aidha katika kuboresha utoaji huduma katika hospitali ya Kibena ambayo kwa sasa inahudumia halmashauri tatu za Wanging'ombe, Makambako na Wilaya ya Njombe; Halmashauri imeingia mkataba wa uendeshaji (MoU) baina yake na Mkoa ili kuimarisha usimamizi na utoaji huduma hadi pale ujenzi wa Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Njombe utakapokamilika. Mkataba tayari umeshasainiwa na pande zote mbili kuanzia tarehe 28/11/2016 hivyo katika kipindi hiki Hospitali ya Kibena itakuwa ikitoa huduma kama hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Njombe kwa kuzingatia makubaliano yaliyomo kwenye Mkataba.

3. MKAKATI KUELEKEA UCHUMI WA KATI WA VIWANDA

Pamoja na maelezo ya awali yenye kuainisha hali halisi ya kiuchumi na kijamii iliyopo katika halmashauri ya mji wa Njombe, maelezo ambayo yanapatikana pia katika kijarida cha wasifu wa uwekezaji cha Mkoa wa Njombe (Njombe Region Investment Profile; Second Edition 2014); Halmashauri ya Mji Njombe kwa kuanzia itajikita zaidi katika kujenga mazingira wezeshi ili kuvutia wawekezaji toka sekta binafsi na mashirika ya umma kwani uwekezaji unahitaji fedha nyingi. Bila kuhusisha sekta binafsi utekelezaji wa mpango huu utachukua muda mrefu kufikia malengo. Hivyo ili kufanikisha mkakati wa kuelekea uchumi wa kati wa viwanda; Halmashauri imetenga maeneo mbali mbali kwa ajili ya uwekezaji katika viwanda na kilimo cha mashamba makubwa.

3.1 Maeneo yaliyotengwa kwa Uwekezaji wa viwanda

Halmashauri imetenga maeneo mbalimbali na baadhi yake yamepimwa kwa ajiri ya kuvutia wawekezaji katika nyanja mbalimbali za uzalishaji katika sekta ya viwanda. Jumla ya ekari **(20)** Kijiji cha Lwangu zimetengwa, kupimwa na kuidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha chai (Unilever Tanzania Ltd); Ekari **(54)** eneo la Yakobi zimetengwa na kupimwa kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha kuunda (assembling) pikipiki, ujenzi wa Chuo cha VET na Kiwanda cha Bati; Ekari **(10.12)** - Nundu kwa ajili ya Kituo cha Kukusanyia na kuhifadha Matunda na Mboga mboga (Sorting, Grading and Packaging) na tayari miundombinu iko hatua za ukamilishaji; Ekari **10.2**. kata ya Uwemba, Mtaa wa Magoda limepimwa kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Mbao (Timber Processing Industry); Ekari **18.72** - Tarafa ya Njombe Mjini, Kata ya Mjimwema limetengwa (bado halijapimwa na kulipiwa fidia) kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo.

Hizi zote ni juhudi za kuongeza idadi ya wananchi hasa vijana na wanawake ambao maisha yao hayatategemea kilimo kwa asilimia kubwa siku za usoni na

hatimaye kuifanya halmashauri ya Mji Njombe iweze kukidhi vigezo vya kuwa manisipaa.

Jedwali Na.1 Maeneo Yaliyotengwa Kwa Ajili Ya Uwekezaji Katika Viwanda Mbalimbali

NA	ENEO LILIPO	UKUBWA WA ENEO	SHUGHULI INAYOTARAJIWA KUFANYIKA	MIUNDOMBINU ILIYOPO	MAELEZO
1	Kijiji cha Lwangu,	Ekari 20.	Ujenzi wa Kiwanda cha Chai	Barabara	Eneo hili limepinwa na limegawiwa/ kumilikishwa kwa mwekezaji kupitia National Land Allocation Committee' na mwekezaji Unilever Tanzania Ltd
2	Kijiji cha Yakobi	Ekari 54.	Eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha kuunda (assembling) pikipiki, ujenzi wa Chuo cha VET na Kiwanda cha Bati.	Barabara, Maji	Eneo limepinwa, lakini bado taratibu za umilikishwaji hazijafanywa kwa kuwa mwekezaji bado hajafika rasmi.
3	Mtaa wa Nundu, Kata ya Yakobi.	Ekari 10.12(mita za mraba 39,916)	Eneo kwa ajili ya Kukusanyia na kuhifadhi Matunda na Mboga mboga (Sorting , Grading and Parking) kabla ya kupelekwa kwenye masoko	Barabara, Maji na Umeme, Jengo la kuhifadhi matunda na nyumba ya Mtumishi	Uwekezaji unafanywa na TAHA kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Njombe.
4	Kata ya Mjimwema	Ekari 18.72	Eneo kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo.	Barabara, Maji na Umeme	Eneo hili bado halijapimwa na bado fidia haijalipwa na bado halijamilikishwa.
5	kata ya Uwemba, Mtaa wa Magoda	Ekari 10.2.	Eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Mbao (Timber Processing Industry)	Barabara, Maji na Umeme	Eneo limepinwa lina ukubwa wa Eneo bado halijamilikishwa na bado halijapata mwekezaji

3.2 Maeneo yaliyotengwa kwa Uwekezaji wa mashamba makubwa

Aidha Kwenye Mpango kabambe halmashauri itazingatia na tayari jumla ya ekari **1,759** zimetengwa mahususi kwa shughuli za kilimo cha mazao ya biashara kama vile Chai na maua ili kuwawezesha wawekezaji kwenye viwanda vya chai kupata malighafi (Uwemba ekari - **850**; Mgala ekari - **402**; Lwangu ekari - **307** na Ng'elamo ekari - **200**).

Jedwali na.2 Maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji katika kilimo cha mazao ya biashara

Na	Eneo lilipo	Ukubwa (ekari)	Shughuli iliyokusudiwa kufanyika	Miundombinu iliyopo	Maelezo
1	Kijiji cha Ng'elamo	200	Kilimo cha mazao ya biashara	Barabara, Maji	Eneo lipo kwenye Mipango ya Halmashauri ya Kijiji
2	Mtaa wa Uwemba	850	Kilimo cha maua	Barabara, Maji na Umeme	Eneo limepinwa
3	Kijiji cha Mgala	402	Kilimo cha Chai	Barabara, Maji	Eneo lipo kwenye Mipango

					ya Halmashauri ya Kijiji
4	Kijij cha Lwangu	307	Kilimo cha Chai	Barabara, Maji	Eneo lipo kwenye Mipango ya Halmashauri ya Kijiji
5	Yakobi	33	Kilimo/shamba la Nyasi	Linafaa kwa nkilimo cha nyasi	Eneo lipo kwenye Mipango ya Halmashauri

Jedwali na.3 FURSA MBALIMBALI ZILIZOPO NA HATUA ZA KIUTENDAJI ZILIZOFANYIKA KWA UJUMLA

SEKTA	FURSA ZILIZOPO	KILICHOFANYIKA HADI SASA KWA KILA FURSA	MPANGO MKAKATI WA SASA NA BAADAE	SHUGHULIZITAKAZOFANYIKA	MUDA WA UTEKELEZAJI	VYANZO VYA FEDHA
Kilimo na ufugaji	Ardhi yenye rutuba na inayofaa kwa kilimo cha kibiashara na ufugaji	Jumla ya ekari 1,759 zimetengwa kwa ajili ya kilimo chamazao ya chakula na biashara (Tazama Jedwali na 2)	Kuimarisha na kuweka miundombinu inyohtajika kama barabara na Maji ifikapo 2018	- Uzalishaji wa chai - Uzalishaji wa matunda - Uzalishaji Maua kwa ajili ya kusafirisha nje - Uzalishaji wa Miti ya mbao na nguzo	2018	Sekta Binafsi
	Kuwepokwa masoko ya kisasa ya bidhaa za kilimo na mifugo	Halmashauri imetenga Fedha kw enye bajeti ya 2016/2017 kwa ajili ya kujenga soko la kisasa la kuuzia viazi na mifugo ili kudhibiti bei	- Kuhamasisha uanzishaji wa mradi mkubwa wa kuzalisha mbegu bora za viazi (uzoefu toka Kilolo) ifikapo 2020 - Kutoa Elimu juu uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo yanavyokidhi viwango katika masoko ya kimataifa kupitia mashamba darasa (FFS) na ugani	Ujenzi wa miundombinu ya soko na minada	2016 -2020	Ruzuku toka serikali kuu (CDG) & Mapato ya ndani
	Kuwepokwa kituo cha kisasa cha kukusanyia matunda katika kijiji cha Nundu	Halmshauri kwa kushirikiana TAHA, Wananchi na sekta binafsi (PPP) imejenga kituo cha kisasa cha Kukusanyia, matunda kuchambua (sorting), kupanga madaraja (grading) na kufungasha (packaging)	- Kutoa Elimu juu uzalishaji wa matunda yanayokidhi viwango katika masoko ya kimataifa kupitia mashamba darasa (FFS) - Kuhamasisha wananchi kulima matunda	Kukusanyia matunda, kuchambua (sorting), kupanga katika madaraja (grading) na kufungasha (packaging) kabla ya kusafirishwa katika masoko ya ndani na nje.	2017	TAHA, SERIKALI KUU
Viwandana Biashara	Kuwepokwa maeneo yanayofaa kwa uw ekezaji wa viwanda vikubwa	Halmshauri imetenga jumla ya ekari 84.2 kwa ajili ya viwanda vikubwa (Tazama Jedwali na. 1)	- Kulipa fidia ya ardhi - Kuweka miundombinu inyohtajika (barabara, Maji na umeme ifikapo Juni 2020	- Ujenzi wa kiwanda cha Chai Lwangu - Ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza Bati - Ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha pikipiki (Assembling) - Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mbao (Processing)	2020	Halmashauri, & Sekta Binafsi
	Kuwepokwa Kiwanda cha kusindika Maziwa (NJOLIFA/CEFA)	Halmashauri inaendelea na ujenzi wa vituo vya kukusanyia maziwa toka kwa wafugaji (Nundu na Itulike)	Kumalizia ujenzi wa kituo cha kukusanyia maziwa cha Nundu na na itulike na kuweka vifaaa vinavyohtajika ifikapo Juni 2017	Ukusanyaji wa maziwa toka kwa wakulima	2017	Mapato ya ndani & CDG
	Kuwepokwa maeneo yanayofaa kwa uw ekezaji katika viwanda vidogo	Halmshauri imetenga jumla ya ekari 18.72 kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo na biashara (Tazama Jedwali na2)	Kufanya upembuzi wa kutambua viwanda vidogo vitakavyo chochea ukuaji wa sekta zingine kama kilimo, mifugo nk ifikapo 2018	Kuongeza mnyororo wa thamani (value chain addition) kwa bidhaa za kilimo, mifugo nk.	2018	Mapato ya ndani & CDG
	Kuwepokwa migodi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga	Kutambua fursa za kibiashara na ajira zitakazopakikana kutokanana na uwekezaji katika miradi ya Mchuchuma na Liganga	Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika maeneo ya utoaji wa huduma kama Mahoteli, usafirishaji nk ifikapo 2020	- Ujenzi wa mahoteli ya kisasa - Ujenzi wa vituo vya kisasa vya biashara (shopping centers)	2020	Sekta Binafsi
	Kuwepo kwa maeneo ya kisasa ya kufanyia biashara	Halmshauri inaendelea na ukamilishaji wa jengo la kufanyia biashara (Pombe Shop) ambalo litachochea ukuaji wa sekta ya biashara na kuongeza wigo wa makusanyo ya ndani	Kuhamasisha sekta binafsi kujenga majengo makubwa ya biashara za aina mbalimbali (kama Mlimani City, West Gate nk) ifikapo 2025	Kuendesha bashara za aina mbalimbali	2025	Sekta binafsi Mapato ya ndani (Own source)
	Upatikanaji wa mitaji yenye masharti nafuu kwa vikundi vya kiuchumi	Fedha kasi cha Sh.277,604,100 zimetengwa katika bajeti ya 2016/2017 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya Vijana na Wanawake	Kutoa mikopo kwa vikundi 160 vya kiuchumi kwa wanawake na vijana kila mwaka	- Shughuli ndogondogo za kiuchumi (IGA) - Kutoa elimu ya ujasiliamali kwa wananchi	Endelevu	Mapato ya ndani
	Kuwepokwa Mpango wa jumla wa Mji (GPS)	Maandalizi ya concepts mbalimbali za ukuaji wa mji ili kupata maoni ya Wadau	Kupima ardhi yote ya halmashauri kwa ajili ya matumizi mbalimbali ifikapo 2020	Kutoa hati miliki za ardhi zitakazo wasaidia wananchi kupata mikopo katika taasisi za fedha kwa ajili ya kuanzisha miradi ya kiuchumi	2025	Ruzuku na Mapato ya ndani